

AGIZO LA AFISA WA AFYA WA MTAALOHITAJI THIBITISHO YA KUPUKEA CHANJO

Kaunti ya King imeendelea kuwa na ongezeko la visa vingi vya COVID-19 na watu kulazwa hospitalini, na kuongezeka kwa vifo vinavyotokana na aina ya virusi vya delta. Visa hivi na vifo vinaweza kuzuiwa kwa kupata chanjo. Kwa hivyo, Afya ya Umma ya Seattle na Afisa wa Afya wa Kaunti ya King Dk. Jeff Duchin walitoa Agizo la Afisa wa Afya wa Mtaalohitaji thibitisho ya kupokea chanjo kamili au matokeo yanayoonyesha mtu hana ugonjwa wa COVID-19 katika baadhi ya hafla za ndani na nje ya majengo na majengo ya biashara. Chanjo ndiyo zana yetu bora dhidi ya kupambana na ugonjwa wa COVID-19.

Sera mpya inajumlisha yafuatayo:

Kuanzia Oktoba tarehe 25, 2021 wateja/watu watahitajika kuonyesha idhibati kuwa wamepokea chanjo ya COVID-19 iliyoidhinishwa na FDA au WHO katika:

- **Shughuli za nje ya majengo** zenye watu mia tano au zaidi (kama vile michezo ya kitaalamu na ya vyuo vya elimu na shughuli/hafla za burudani)
- **Shughuli za burudani za ndani ya majengo au maeneo ya biashara** bila kuzingatia idadi ya watu (kama vile michezo ya kitaalamu na ya vyuo vya elimu, maeneo ya maigizo ya kisanaa na muziki unaochezwa moja kwa moja, kumbi za sinema, maeneo ya mazoezi, na maeneo ya mikutano)
- **Mikahawa na baa.** Hii inatumika kwa maeneo ya ndani ya majengo ya watu kulia. Haitumiki kwa maeneo ya nje ya majengo ya watu kulia, maeneo ya wateja wa kununua na kubeba vyakula, na maeneo ambayo hayatumiwi sana kama maeneo ya ndani ya majengo ya kulia kama vile maduka ya mboga. Agizo hili linatoa nafasi kwa mikahawa midogo na baa ambazo zina uwezo wa kuwa na watu kumi na wawili au chini yake muda zaidi kujipanga, kwani litaanza kufanya kazi Disemba tarehe 6.

Ni nini inazingatiwa kama idhibati kuwa umepokea chanjo?

- Kadi ya rekodi ya chanjo ya COVID-19 ya CDC COVID-19 au picha ya kadi ya chanjo
- Cheti kilichochapishwa au kodi ya QR (itapatikana mwisho wa mwezi wa Septemba) kutoka kwa tovuti ya [MyLRMobile.com](https://mylr.com) (tovuti inapatikana kwa lugha ya kiingereza pekee)
- Rekodi nyingine rasmi za chanjo kutoka ndani au nje ya Marekani, Pamoja na inayotoka kwa mhudumu wako wa afya. Picha au nakala ya kadi hii iliyorudufiwa pia inakubalika.

KUMBUKA: Stakabadhi za kimatibabu au kidini zinazoonyesha sababu ya mtu kutopewa chanjo **hazikubaliki. Huhitaji** kuonyesha kitambulisho Pamoja na idhibati ya kuwa umepokea chanjo.

Chaguo kwa wale ambao hawajachanjwa au hawawezi kuthibitisha hali yao ya chanjo

Watu ambao hawajachanjwa au hawawezi kuthibitisha hali yao ya chanjo lazima waonyeshe idhibati ya:

- matokeo yanayoonyesha hawana ugonjwa wa COVID-19 kutoka kwa vipimo vinavyotafuta nyenzo ya maumbile kutoka kwa virusi vya Corona (PCR) iliyofanywa masaa sabini na mawili yaliyopita au matokeo ya haraka kutoka kwa vipimo vilivyofanywa na mtoa huduma wa vipimo papo hapo katika hafla kabla tu ya kuingia.

Majengo ya biashara yatawajibikia kuangalia idhibati ya chanjo au hali ya matokeo yanayoonyesha mtu hana ugonjwa wa COVID-19. Afya ya Umma itafanya kazi na washirika ili kutoa msaada wa kiufundi na vifaa vya elimu kwa biashara na mashirika yanayotekeleza agizo hili.

Utengenezaji wa Sera

Kaunti ya King na Afya ya Umma ziliunda sera hii kwa kushauriana na Kikundi cha Janga la Afya ya Umma na ushauri wa jamii kuhusu ubaguzi wa rangi, miji, biashara ndogondogo, makundi yanayolinda masilahi ya wanabiashara, vyama vya wafanyakazi, makundi ya kibiashara, timu za michezo, kumbi, makundi ya kijamii, viongozi wa kidini kutoka kote katika Kaunti. Wanalenga kutengeneza kile ambacho kinaweza kufanya kazi, kwa haki, na usawa kwa wanabiashara na wakazi.

Kwa habari zaidi, tembelea tovuti ya: kingcounty.gov/verify (rasilimali zilizotafsiriwa zinapatikana)